

Oktoba 2016



Marafiki wapendwa,

Ni heshima kuungana na nyinyi kwenye mchakato huu wa maombi ulimwenguni. Wewe ni sehemu muhimu sana ya timu yetu ya maombi kimataifa ya Project Hannah. Upendo na maombi yako ni ya muhimu sana kwetu na yanahitajika sana kwenye nyakati kama hizi!

Mioyo na fahamu zetu zinapoungana mwezi huu wa kumi, ninatamani kila mmoja wetu kutafakari kwa njia ya maombi maana ya kuwa na kiu na njaa kwa ajili ya Mungu. Kumjua zaidi, kumsifu zaidi, na kumkimbilia ili kupata tumaini na uponyaji tunapokuwa tunaumia. Kupata kitu mnachotamani sana kwenye maisha yetu kuwa muumbaji, aliyeziumba nafsi zetu.

Naamini wanawake wenye njaa zaidi kwa ajili ya Mungu wanaweza kubadilisha ulimwengu kwa ajili ya Yesu. Hata hivyo, ili tuweze kuwa na maisha hayo, ni lazima tudhamirie kuchukua hatua kwa mambo ya Mungu yatakayoziridhisha nafsi zetu. Tunapopata njaa kubwa ya Mungu kupitia maombi, ni lazima tutengeneze nafasi maishani mwetu zaidi kwa ajili ya Mungu.

Yesu alisema, “Heri wenye njaa na kiu ya haki; Maana hao watashibishwa,” (Mathayo 5:6). Sasa kwa nini hatuoni zaidi uwezo wa Mungu na uwepo wake leo? Jibu ni rahisi sana: Tumejazwa na vitu vingi ambavyo si vya Mungu.

Nimejiuliza, “Kuna mambo kwenye maisha yangu ambavyo ni lazima nimpe Yesu ili kutengeneza nafasi zaidi kwa ajili ya uwepo na uwezo wa Mungu? Je, nina njaa ya ziada kwa ajili ya Mungu? Niliwahi kumsikia mwanamke akiuliza swali, “Nawezaje kuwa mwanamke mcha Mungu?” Jibu langu lilikuwa, ili kuwa mwanamke mcha Mungu, unamhitaji Mungu zaidi.

Tunahitaji uwepo na uwezo wake kwenye maisha yetu. Tunatakiwa kuwa na njaa na kiu ya haki, haki inayotokana na mahusiano yetu na Yesu. Tunapotamani kuwa na uhusiano wa ndani zaidi, tunajazwa na kuridhika.

Swali ni kwamba, “Una njaa ya kumpata Mungu zaidi?” Una njaa ya kutosha kumkimbilia Mungu na kumlilia kwa sababu yeye ndiye suluhisho lako la pekee kwa uponyaji na matunzo yako ya kiroho?

Nina hamu ya kuwa na njaa na kiu ya kiroho ya kila siku. Ninaamini na wewe pia. Maombi yetu ya mwezi huu na yawahamasishe wengine wawe na njaa ya kuwa na uhusiano wa karibu na Mungu kupitia kwa Mungu kupitia kwa Bwana wetu Yesu Kristo!

Katika yeye mioyo yetu inashangilia,

Peggy Banks
Mkurugenzi wa Kimataifa wa Huduma
Project Hannah